# STD 8 END TERM 2 EXAM 2019

## KISWAHILI

2. Hakikisha ya kwamba yafuatayo umeandika katika karatasi ya majibu:

I) JINA LAKO                II) JINA LA SHULE YAKO

***Jaza nafasi 1 - 15 kwa kutumia jibu sahihi kwa kukamilisha nafasi zilizoachwa wazi.***

Dunia __1__ rangi __2__. Walimwengu __3__ ulimwengu __4__ hawaishi kunishangaza kila kuchao. Namna tunavyozidi kuishi katika ulimwengu huu __5__ tunavyozidi kushuhudia mmomonyoko wa __6__ na __7__ wakitiririka katika utepe __8__ wa __9__ ya uwajibikaji. Ama ndiyo dunia ya kila mwamba ngozi __10__ kwake __11__ Hata hivyo, __12__ kuvutia __13__ sharti kuwe na mipaka na __14__ unaoambatana na __15__ katika jamii.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. kweli | B. ni | C. si | D. ama |
| 2. | A. nyekundu | B. kijani | C. nyeusi | D. rangile |
| 3. | A. juu | B. wenye | C. katika | D. kati |
| 4. | A. hii | B. huu | C. hizi | D. humu |
| 5. | A. ndiyo | B. ndivyo | C. ndivo | D. ndizo |
| 6. | A. udongo | B. madili | C. maadili | D. utu |
| 7. | A. mengi | B. nyingi | C. wingi | D. wengi |
| 8. | A. moja | B. mmoja | C. kimoja | D. umoja |
| 9. | A. upuzi | B. puuza | C. mapuuza | D. ubishi |
| 10. | A. hukata | B. hukaza | C. huvuta | D. hupaka |
| 11. | A. ? | B. ! | C. . | D. , |
| 12. | A. huko | B. huku | C. humu | D. hapa |
| 13. | A. kwako | B. kwao | C. kwako | D. kweto |
| 14. | A. mitaro | B. utu | C. umma | D. undugu |
| 15. | A. hujuma | B. thima | C. dhima | D. heshima |

***Kutoka swali la 16 - 30, chagua jibu lililo sahihi kulingana na maagizo uliyopewa.***

16. Kitenzi shuka katika kauti ya kutendesha ni
    A. shukisha    B. shusha
    C. shukiza    D. teremusha

17. ***Andika kinyume cha:-***
    Mama amevimba mkono
    A. Baba amepwea mkono
    B. Mke amepwea mkono
    C. Baba amepwea mguu
    D. Mke amepwea mguu

18. Mvua ya manyunyu huitwa
    A. mvua ya matone
    B. mvua ya mawanga
    C. mvua ya kipupwe
    D. mvua ya vuli

19. Chagua nomino ambayo haiwezi patikana katika nomino **jenga**.
    A. Mjenzi
    B. Ujenzi
    C. Kujenga
    D. Mjengi

20. Chagua jina la makundi lisilo sahihi.
A. Kipeto cha barua
B. Bumba la nyuki
C. Ufefe wa mahindi
D. Funda la ugali

21. Neno **haina** lina maana sawa na
A. toroka B. gura
C. ambata D. toweka

22. Jina la jumla la nyani, tumbiri na sokwe ni
A. kima B. kuchi
C. gundule D. kiradi

23. Jina la sayari ya tano ni ________
A. mshtari B. kausi
C. mirihi D. zuhura

24. ***Kanusha;***
Wewe umenenepa.
A. Mimi sijanenepa
B. Wewe hujanenepa
C. Wewe umekonda
D. Sisi tumekonda

25. Ndewe kwa sikio, ufizi kwa ________
A. kichwa B. mdomo
C. mkono D. mguu

26. Neno mkuki liko katika ngeli ipi?
A. U - I B. U - U
C. U - ZI D. LI - YA

27. Kamilisha methali;
Uzuri wa mkakasi ndani
A. zaibaki B. dhahabu
C. chuma D. kipande cha mti

28. Maziwa haya ________ niliyoyanywa.
A. ndizo B. ndilo
C. ndiyo D. ndio

29. Uso hufanywa nini ________
A. hunawa B. huoshwa
C. huoga D. hupakwa

30. Kisawe cha neno ugali ni
A. sima B. ufefe
C. unga D. pojo

***Soma habari hii kisha ujibu maswali 31 - 40.***

Mgogoro ulizuka kazini pa Kaku. Kiasi kikubwa cha pesa kilipotea kwa njia ambayo haikuweza kuelezeka. Kwa sababu Kaku alikuwa mhasibu mkuu, alihusishwa na kashfa hiyo. Alimwaga unga na kushtakiwa. Alijaribu kujitetea kuwa hakuhusika kwa vyovyote vile na kuapa mbele ya hakimu. Kama tujuavyo siku ya kufa nyani, miti yote huteleza. Ushahidi uliotolewa ulimpata na hatia kubwa. Aliambiwa alipe shilingi milioni tano au afungwe kwa miaka miwili gerezani. Alichukua akiba yake yote pamoja na mkopo wa benki na kulipa faini. Aliachiliwa huru lakini alibaki hana hanani. Maisha ya ukata yaliwavamia vaa bin vuu. Upendo kwenye familia ulianza kudidimia polepole na hatimaye kutoweka kabisa. Kilichosalia ni ugomvi, rabsha na dharau.

Siku moja, mke wake alisikika akimtusi mume wake mchana wa jua. "Mwanaume gani wewe? Mtu asiye na uwezo wa kutunza familia yake ajiita mwanaume? Upuuzi mtupu huo." Bwana Kaku hakuweza kujibu kwa sababu hakuwa na jibu. Matusi yaliendelea na mwishowe aliamua kumtaliki mke wake. Mke alipokea talaka kwa furaha na kuondoka akimwachia mwanawe. Ukiwa ulimsonga lakini baadaye alimpata mke mwingine aliyempenda bila kujali umasikini wake. Aliamini kuwa elimu ni ngao. Mke alimpenda mtoto wa Bwana Kaku kama mwana wake. Akiwa mjamzito, bwana Kaku alifanikiwa kupata kazi nyingine kama mkurungenzi wa fedha katika benki moja. Maisha yalibadilika tena. Kumbe alikuwa ameteleza tu na kuteleza si kuanguka. Aidha kujikwaa si kuanguka bali ni kusonga mbele. Mke wake alimzalia wana watatu. Binti mmoja na bin wawili. Waliishi maisha ya upendo wa dhati. Fanaka zao zilienea kama moto jangwani na kumfikia mke wa kwanza. Alirudi kwa bwana Kaku na kumwomba msamaha akiomba amrudie mume wake wa zamani. Bwana Kaku alimsamehe kwa dhati ya moyo wake lakini akamjulisha kuwa nafasi yake haikuwa pale.

Aliondoka akibubujikwa na machozi huku akisadiki kuwa majuto ni mjukuu huja kinyume na pia, upendo haujengwi kwa sababu ya mali bali pia wakati wa shida. Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki.

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

31. Ni nini kilichosababisha mgogoro kwenye kazi pa Kaku?
A. Shida ya kifamilia
B. Ukosefu wa fedha
C. Wateja hawakuonekana
D. Pesa zilizopotea kwa njia tata

32. Bwana Kaku alikuwa amesoma nini?
A. Kazi ya uandizi
B. Kazi ya walimu
C. Kawi ya uuguzi
D. Kazi ya hesabu ya kifedha

33. "Alimwaga unga," ni fani gani ya lugha ya
A. istiara
B. nahau
C. tashbihi
D. tasfida

34. Miti ya bwana Kaku uliteleza kivipi?
A. Kupata talaka
B. Kumwaga unga
C. Kupoteza kazi
D. Kula kalenda

35. Ni nini kilichomfanya bwana Kaku kufilisika?
A. Kufuata kazi
B. Biashara kucharibika
C. Faini aliyolipa
D. Talaka

36. Maisha ya ukata ni maisha gani?
A. Ukwasi
B. Umaskini
C. Uadilifu
D. Upole

37. Ni nini kilichokuwa chanzo cha ugomvi katika familia?
A. Mke mkaidi
B. Mume kaidi
C. Ukosefu wa pato
D. Mke wa pili alikuwa chanzo

38. Matusi na madharau yaliyotolewa na mke wa bwana Kaku ilikuwa ishara tosha kuwa
A. alikuwa mkali
B. alimdharau mume wake
C. upendo wake ulikuwa wa kipesa
D. alikuwa hawara

39. Mke wa pili alikuwa _______ kwa mwana wa bwana Kaku.
A. Halati
B. Shangazi
C. Mama mdogo
D. Mama wa kambo

40. Neno <u>aidha</u> limetumika katika habari. Lina maana gani?
A. Tena
B. Pia
C. Nia
D. Lakini

***Soma habari hii  kisha ujibu maswali 41 - 50.***

Kuna vitu ambavyo hauwezi kuvipata kwa sababu una mali mengi. Staarabu, hekima na afya bora ni majaliwa kutoka kwa muumba. Hospitali za kifahari zimejaa wakwasi. Kando na uchungu wa kuugua, wanahofia kuacha mali yao. Ugonjwa pamoja na woga hatima yake ni mauko.

Ukwasi unaoleta furaha ni ule ambao umepatikana kwa kutoa jasho. Ukiwa mchumia juani unapolia uvulini utakuwa umetulia na kuterema. Usiku utaleta usingizi wa pono bila jinamizi. Kwa upande mwingine, ukwasi uliotafutwa kwa njia za hila hauleti furaha. Mchana kutwa na usiku kucha ni tabu. Huogopa pengine aliowatapeli mali yao huenda wakapanga njama ya kumwangamiza. Usingizi kupata ni shida na aupatapo hukaribishwa na jinamizi. Kwingineko mtu mwenye mapato ya chini hutaabika mchana akijitafutia akiwa na matumaini kuwa ipo siku ambayo atafanikiwa. Afikapo nyumbani usiku, usingizi humlemea na kulala fofofo. Njozi zake huwa za matumaini. Anaweza kuota akiwa mfalme, mkwasi au kwenye sherehe akigwengwenya minofu ya nyama au ameandaliwa chakula kilichojaa chinyango. Tatizo ni kuwa ruiya haiwezi kukuruhusu kula. Unapojiandaa kupeleka chakula mdomoni, umeamka. Umeamka ukilala tena, ndoto haijiendelezi, pengine ianze nyingine.

**41.** Kutokana na makala haya, vitu hivi hauwezi kupata kwa ukwasi wako ila
A. ustaarabu B. hekima
C. pesa D. afya

**42.** Katika aya ya kwanza, matajiri wanapolazwa hospitalini huofia kuhusu
A. kifo
B. jamaa na jamii zao
C. wake zao
D. kuacha mali

**43.** Ugonjwa na uoga huleta
A. maradhi
B. kulazwa
C. mauti
D. hekaheka

**44.** Mali mazuri ambayo mtu hustahili ni yapi?
A. Uliochiwa na wazazi
B. Alipata kanisani
C. Aliofanyia bidii
D. Mali yeyote

**45.** Methali ipi ina maana sana na "mchumia juani hulia uvulini."
A. Mtegemea nundu hakosi kunona
B. Achanikiaye kwa mpini hafi kwa njaa
C. Ajizi ajizi ni nyumba ya njaa
D. Mla leo toa tugawe

**46.** Kinyume cha usingizi jinamizi ni ipi?
A. Mang'amung'amu
B. Kwikwikwi
C. Pono
D. Furaha

**47.** Kivuli kinachomfuata mtu aliyepata mali yake kwa ila ni
A. Furaha
B. Huzuni
C. Watu aliyewatapeli
D. Maadui wake

**48.** Kitu gani ambacho mtu wa pato la chini amebarikiwa nacho?
A. Usingizi B. Imani
C. Tumaini D. Upendo

**49.** Ndoto humsaidia vipi mkata?
A. Humpa usingizi
B. Humpa mali
C. Humpa matarajio ya kufanikiwa siku zijazo
D. Humpa amani na raha

**50.** "Tatizo ni kuwa ruiya haiwezi kukuruhusu kula. Unapojiandaa kula, ndoto hukatika. Ina maana kwamba
A. ndoto hasa huwa ndefu sana
B. ndoto huwa ni nyingi mno
C. ndoto humburudisha tu mkata
D. zile ndoto hazikamiliki wala kutimilika